# KANUNI ZA MAADILI YA MASOKO YA REJAREJA YA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

© Octoba 2023

BENKI KUU YA TANZANIA

# YALIYOMO

**DIBAJI** 1

**SURA YA KWANZA: MAADILI** ........ 2

**1.1. Utangulizi** ........ 2

**1.2. Viwango vya Weledi** ........ 2

**1.3. Viwango vya Maadili** ........ 3

**1.4. Mgongano wa Maslahi** ........ 4

**SURA YA PILI: UIDHINISHAJI WA MIAMALA YA BIASHARA YA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI** ........ 6

**2.1. Utangulizi** ........ 6

**2.2. Upangaji wa Bei** ........ 6

**2.3. Uwasilishaji wa Taarifa za Miamala ya Masoko ya Rejareja ya Kubadilisha Fedha za Kigeni** ........ 6

**2.4. Kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni nje ya eneo la kufanyia biashara** ........ 7

**2.5. Utaratibu wa Utawala katika Shughuli za Kubadilisha Fedha za Kigeni** ........ 7

**SURA YA 3: VIWANGO VYA JUMLA** ........ 8

**3.1. Viwango vya kumtambua mteja na kuzuia utakasishaji fedha haramu na kupambana na ufadhili wa ugaidi** ........ 8

**3.2. Utatuzi wa Malalamiko** ........ 8

**3.3. Uzingatiaji wa Kanuni ya Maadili ya Masoko ya Rejareja ya Kubadilisha Fedha za Kigeni** ........ 9

# DIBAJI

Benki kuu ya Tanzania inasimamia sehemu kubwa ya Sekta ya Fedha nchini Tanzania ikijumuisha usimamizi wa biashara ya fedha za kigeni. Kanuni za Maadili kwa Masoko ya Rejareja ya Fedha za kigeni zimeandaliwa ili kuweka viwango vinavyokuza uadilifu na ufanisi wa soko la rejareja la fedha za kigeni nchini Tanzania. Kanuni za masoko ya rejareja ya fedha za kigeni itawezesha utendakazi mzuri wa biashara kwenye soko la rejareja la fedha za kigeni inayofanywa na benki, taasisi za fedha, na maduka ya kubadilisha fedha nchini Tanzania.

Kanuni za Masoko ya Rejareja ya Fedha za Kigeni zimetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 7(1)(b) cha Sheria ya Fedha za Kigeni, Sura ya 271 ambayo inaipa Benki Kuu mamlaka ya kutoa maelekezo kuhusu utaratibu unaopaswa kuzingatiwa na taasisi au mtu yeyote anayefanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni nchini Tanzania.

Madhumuni ya Kanuni hizi ni kuweka viwango na utaratibu mzuri kwa washiriki wa soko la rejareja wanaposhiriki katika miamala ya ubadilishaji wa fedha za kigeni na umma kwa ujumla au miongoni mwao wenyewe. Kanuni hizi zitatumika kwa benki, taasisi za fedha na maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yanayojihusisha na biashara ya rejareja ya kubadilisha fedha za kigeni nchini Tanzania.

Emmanuel M. Tutuba
APPROVED
Oct 15 2023 1:14 PM
DocuSign

Gavana

Benki Kuu ya Tanzania

Oktoba, 2023

# SURA YA KWANZA: MAADILI

## 1.1. Utangulizi

Soko la rejareja la kubadilisha fedha za kigeni lina mchango mkubwa katika uingizaji wa fedha za kigeni katika uchumi kwa kutoa fursa ya kununua na kuuza fedha za kigeni papo kwa papo kwa wateja wa rejareja, hivyo kuchangia uwepo wa bei halisi sokoni. Kutokana na umuhimu wake, washiriki wa soko wanatarajiwa kudumisha maadili na weledi ili kukuza usawa na uadilifu wa Soko la rejareja la kubadilisha fedha za kigeni. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuzingatia uadilifu na weledi katika kufanya maamuzi, washiriki wa soko la rejareja wanapaswa kuongozwa na misingi ya uadilifu wanaposhiriki soko fedha za kigeni.

Washiriki wote wa soko wana maslahi ya pamoja katika kudumisha kiwango cha juu cha weledi na maadili katika kufanya biashara kwenye Soko la rejareja la kubadilisha fedha za kigeni.

Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, "mshiriki wa soko" ni benki au taasisi ya fedha au duka la kubadilisha fedha za kigeni ambalo linashiriki katika soko la rejareja la kubadilisha fedha za kigeni kama sehemu ya kawaida ya biashara yake na linashiriki katika biashara ya kununua au kuuza fedha, au katika miamala inayopelekea kupata faida au hasara kulingana na mabadiliko katika kiwango cha Kubadilisha fedha za kigeni.

## 1.2. Viwango vya Weledi

Katika kufanya miamala ya kubadilisha fedha za kigeni, washiriki wa soko wanapaswa:

(a) kuwa na uangalifu wa kutosha;

(b) kutumia lugha iliyo wazi na isiyokuwa na utata;

(c) kuonesha bei kwenye ubao uliowekwa mahali panapo onekana katika eneo la biashara;

(d) kufichua masharti na vigezo vinavyotumika katika miamala ya kubadilisha fedha za kigeni;

(e) kuonesha ada na gharama za miamala ya kubadilisha fedha za kigeni mahali panapo onekana;

(f) kuanzisha na kutekeleza miundo ya utawala, sera, taratibu, vidhibiti vya ndani, rasilimali, na mpango wa mafunzo ili kuhakikisha Kanuni za Maadili ya Masoko ya Rejareja ya Kubadilishia Fedha za Kigeni zinazingatiwa;

(g) kuwa na uelewa wa kutosha wa sheria zinazo husika;

(h) kuwa na uzoefu wa kutosha na maarifa yanayohusiana na uendeshaji wa shughuli za soko la Rejareja la Kubadilisha Fedha za Kigeni;

(i) kufanya biashara kwa ustadi na ujuzi;

(j) kutumia weledi katika kuzingatia miongozo ya uendeshaji wa soko na taratibu za uendeshaji ikijumuisha na njia za utekelezaji, kuhifadhi kumbukumbu na mienendo mizuri ya maadili; na

(k) kujiepusha na tabia au mwenendo wowote unoweza kushusha hadhi ya Soko.

## 1.3. Viwango vya Maadili

1.3.1. Washiriki wa Soko wanatakiwa kudumisha viwango vya juu vya maadili katika kufanya biashara kwenye Soko la Rejareja la Kubadilisha Fedha za Kigeni:

(a) kuwa mwaminifu kwa wateja na washiriki wengine wa Soko;

(b) kutenda haki kwa wateja na washiriki wengine wa Soko bila kutetereka na kwa uwazi;

(c) kuwa na maadili hasa kujiepusha na mienendo na tabia zenye mashaka;

(d) kuwa wakweli kwenye taarifa zao;

(e) kujiepusha na njama za kupanga viwango vya bei;

(f) kujizuia kuchukua hatua za kujinufaisha wao wenyewe au wateja wao kutokana na vitendo vifuatavyo visivyofaa:

(i) kueneza uvumi ambao unaweza kuleta athari kubwa katika weledi; na

(ii) kujaribu kupata taarifa za siri ambazo zinaweza kuwa na athari hasi katika mwenendo wa bei.

(g) Kuzingatia usiri kwa msingi kwamba:

(i) Mshiriki haruhusiwi kutoa au kuvujisha taarifa yoyote inayohusu miamala ya wateja au taarifa nyingine zinazohusiana na akaunti ya mteja kwa mtu mwingine yoyote isipokuwa kama itahitajika kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria;

(ii) Kila mshiriki anapaswa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu misingi ya utunzaji siri na kuchukua hatua zinazohitajika kuzuia nyaraka za siri kuvuja na kwenda kwa watu wasiohusika;

(iii) Washiriki watahakikisha kwamba usiri hauvunjwi kwa sababu ya matumizi ya mifumo ya teknolojia ya mawasiliano au vinginevyo na kwamba hatua stahiki zinawekwa ili kuimarisha ulinzi wa taarifa.

1.3.2. Kudumisha viwango vya juu vya maadili na weledi ni wajibu wa:

(a) Washiriki, unaolenga kukuza maadili na tabia njema ndani ya taasisi, jitihada saidizi zinazokuza viwango vya maadili katika soko lenye wigo mpana na kuhimiza ushirikishwaji wa watumishi katika jitihada hizo;

(b) Maafisa waandamizi na Menejiment ya juu, kwa kuwa tayari kuingiza na kuwezesha tamaduni na maadili mema ndani ya utamaduni wa taasisi na kujiweka tayari kutoa ushauri unaofaa kwa watumishi; na

(c) Mtumishi, kutumia weledi wake anapokabiliana na masuala ya kimaadili. Mtumishi atatakiwa kuomba ushauri pale inapohitajika, kutoa taarifa na/au kupeleka masuala yote muhimu kwa wahusika wa ndani au nje ya taasisi.

## 1.4. Mgongano wa Maslahi

1.4.1. Washiriki wa Soko wanatakiwa kuweka wazi mgongano halisi wa maslahi na unaotarajiwa ambao unaweza kuathiri uwezo wa kufanya maamuzi yao au kuchukuliwa kuwa unaweza kuathiri uwezo wa kufanya maamuzi kwa weledi. Washiriki wa Soko watatakiwa kuondoa migongano hiyo ya maslahi au kama haiwezekani, kuweza kuidhibiti ili kukuza usawa katika kuwahudumia wateja wao na washiriki wengine wa Soko ikiwa ni pamoja na kujizuia kushiriki katika shughuli au tukio kutokana na mgongano wa maslahi uliopo.

1.4.2. Washiriki wa soko watatakiwa kuweka taratibu mwafaka na madhubuti za kuondoa au kudhibiti mgongano wa maslahi ikiwa ni pamoja na:

(a) Kutenganisha majukumu na ngazi za uwajibikaji;

(b) Kuanzisha vizuizi vya utoaji wa taarifa;

(c) Kubadilisha majukumu ya mtumishi pale ambapo majukumu hayo yanaweza kupelekea mgongano wa maslahi;

(d) Kutoa mafunzo kwa watumishi wanaohusika ili kuwawezesha kubaini na kukabiliana na masuala ya mgongano wa maslahi;

(e) Kuanzisha sera za kutangaza migongano ya maslahi na mahusiano binafsi pamoja na zawadi na takrima zinazopokelewa na kuwa na sera na vidhibiti vya masuala binafsi.

1.4.3. Pale itakapothibitika kwamba suala fulani la mgongano wa maslahi haliwezi kuzuilika au kudhibitiwa (ikiwa ni pamoja na kuacha kutoa huduma au shughuli), washiriki wa soko watatakiwa kutoa taarifa toshelezi za mgongano uliopo ili kuwezesha waathirika kuamua kabla iwapo wanataka kuendelea na muamala au la.

## SURA YA PILI: UIDHINISHAJI WA MIAMALA YA BIASHARA YA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

### 2.1. Utangulizi

Washiriki wa Soko wanatarajiwa kuchukua tahadhari wanapofanya majadiliano na kuidhinisha miamala ili kukuza usawa na uwazi katika Soko.

### 2.2. Upangaji wa Bei

(a) viwango vya bei katika soko la rejareja havipaswi kuzidi bei zilizopangwa na kuandikwa kwenye ubao;

(b) washiriki wa soko wanatakiwa kuhuisha viwango vyao vya bei ya kubadilisha fedha za kigeni kwenye ubao baada ya mabadiliko ya bei;

(c) viwango vya kubadilisha fedha za kigeni vinapaswa kuwa ndani ya wigo wa asilimia 4 ya kiwango cha manunuzi.

### 2.3. Uwasilishaji wa Taarifa za Miamala ya Masoko ya Rejareja ya Kubadilisha Fedha za Kigeni

Taarifa za miamala ya kubadilisha fedha za kigeni za washiriki wa Soko zitatakiwa kuonesha:

(a) jina la mteja wa rejareja;

(b) aina ya mteja;

(c) aina ya muamala;

(d) sekta inayohusika na muamala, aina ya fedha iliyofanyiwa muamala, na kiasi cha muamala;

(e) kiwango cha kubadilisha fedha; na

(f) mpangilio wa bei.

## 2.4. Kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni nje ya eneo la kufanyia biashara

(a) Washiriki wa soko wanatakiwa kutojihusisha na biashara ya kubadilisha fedha za kigeni nje ya eneo la biashara lililoidhinishwa na Benki Kuu;

(b) Menejimenti itaweka vidhibiti kuhakikisha inazuia kufanya biashara nje ya eneo la biashara.

## 2.5. Utaratibu wa Utawala katika Shughuli za Kubadilisha Fedha za Kigeni

Washiriki wa soko wanatarajiwa kuwa na mfumo wa utawala thabiti na wenye ufanisi ambao unatoa wajibu, uangalizi wa shughuli zao za Soko la Kubadilisha Fedha za Kigeni la Rejareja, na kuhamasisha ushiriki wa kuwajibika katika Soko la Kubadilisha Fedha za Kigeni la Rejareja.

# SURA YA 3: VIWANGO VYA JUMLA

## 3.1. Viwango vya kumtambua mteja na kuzuia utakasishaji fedha haramu na kupambana na ufadhili wa ugaidi

Washiriki wa soko wanatakiwa kuzingatia matakwa yote ya udhibiti yaliyotolewa na Benki Kuu. Sera na taratibu za ndani za washiriki wa soko zinatakiwa kuendana na matakwa yote ya kisheria na kiusimamizi ikiwa ni pamoja na:

(a) kuweka vidhibiti madhubuti ili kutekeleza kanuni za utambuzi wa mteja, kuzuia utakasishaji fedha haramu na kupambana na ufadhili wa ugaidi;

(b) ufahamu wazi wa sheria na kanuni zote zinazohusiana na kuzuia utakasishaji fedha na kupambana na ufadhili wa ugaidi;

(c) kuweka taratibu za ndani ili kuwezesha utambuzi na utoaji wa taarifa kwa haraka wa shughuli zenye mashaka;

(d) kutoa mafunzo stahiki ya mara kwa mara kwa watumishi, ili kuongeza uelewa kuhusu uzito wa majukumu na wajibu wa kutoa taarifa; na

(e) kufanya mapitio huru ya mara kwa mara kwa kutumia wataalamu wa masuala husika.

## 3.2. Utatuzi wa Malalamiko

Biashara ya kubadilisha fedha za kigeni inaweza kupelekea malalamiko kati ya washiriki wa soko na wateja wao wa rejareja. Hivyo, washiriki wa soko wanatakiwa:

(a) kuanzisha na kutekeleza taratibu za kushughulikia malalamiko ya wateja;

(b) kutoa njia za siri kwa wateja za kutoa malalamiko yao kuhusu matendo na tabia zisizofaa; na

(c) kuchunguza malalamiko na kutoa majibu kwa maandishi kwa walalamikaji ndani ya siku tano za kazi.

Ikiwa malalamiko ambayo uamuzi wa mwisho hauwezi kufikiwa ndani ya kipindi kilichotajwa, Benki Kuu itakuwa na uamuzi wa mwisho kuhusu suala hilo.

### 3.3. Uzingatiaji wa Kanuni ya Maadili ya Masoko ya Rejareja ya Kubadilisha Fedha za Kigeni

Benki Kuu inaweza kuchukua hatua stahiki za kusimamia utekelezaji na hatua nyingine za kiutawala dhidi ya washiriki wa soko ambao watashindwa kuzingatia matakwa ya Kanuni hizi.